

2015

UWEZO TANZANIA



**Mwongozo
wa Wahojaji**
WA KUJITOLEA



UWEZO ni...



- Neno la Kiswahili lenye maana ya 'kipawa/umahiri'
- Jitihada inayoongozwa na wananchi
- Inafanya kazi kote Afrika Mashariki (Kenya, Tanzania na Uganda)
- Inatathmini watoto katika stadi za msingi za kusoma na kuhesabu
- Inakusanya taarifa kutoka shuleni na katika kaya
- Jitihada ya Uwezo imekuwa inatekelezwa na wananchi wa kawaida katika makazi ya jamii zao
- Inawatia hamasa wananchi kuchukua hatua ya kuboresha viwango vya kujifunza vya watoto wao

Dhana ya Uwezo ni rahisi sana. Tunapeleka watoto shule kwa sababu tunatarajia watajifunza stadi za msingi na ujuzi muhimu utakaopelekea ustawi. Hivyo, Uwezo - badala ya kuelekeza nguvu katika idadi ya kuvutia ya madarasa yaliyojengwa, walimu walioajiriwa, na vitabu vilivyotolewa inauliza swali rahisi 'Je, Watoto wetu wanajifunza?'

Tathmini ya Uwezo ya Kitaifa ina vipengele muhimu vifuatavyo:


- Ni ya kitaifa
- Inatumia zana rahisi zilizo rahisi kuelewa
- Inaendeshwa na wananchi wa kawaida
- Inatoa mrejesho wa matokeo papo kwa papo kwa mtoto na mzazi
- Tathmini ya Uwezo hufanyika kila mwaka
- Nitathmini ya kikaya
- Inaangazia stadi za msingi katika kusoma na fufanya hisabati

Uwezo ni juhudi inayofanya kazi eneo la Afrika Mashariki kutathmini viwango halisi vya watoto kwenye stadi za msingi za kusoma na kuhesabu. Ushahidi unaokusanywa hutmika kubadili mwelekeo kutoka mlengo wa kujikita kwenye miundombinu na uandikishaji kwenda mlengo wa kujikita kwenye ngazi halisi za kujifunza za watoto.

CONTENTS

SURA YA 1: KUHUSU UWEZO NA MCHAKATO WAKE	5
SUARA YA 2: KUELEZEA MCHAKATO WA UTAFITI	8
SUARA YA 3: KUTEMBELEA SHULE	10
SURA YA 4: KUTEMBELEA KAYA	12
SURA YA 5: KUWAPIMA WATOTO	14
SURA YA 6: UFAFANUZI WA TATHMINI ZA KUSOMA NA HISABATI	15
SURA YA 7: KUPIMA MZINGO WA MKONO (MUAC)	19
SURA YA 8: KUPIMA MADINI JOTO KATIKA CHUMVI	21
SURA YA 9: MREJESHO WA PAPO KWA PAPO	22
SURA YA 10: MASUALA YA KIMAADILI	24
SURA YA 11: KUHFADHI TAKWIMU BAADA YA TATHMINI	26

ZITAMBUE NEMBO ZAKO



Dhana kuu

Unapooona picha hii, maana yake ongeza umakini kwa kuwa hili ni jambo muhimu kukumbuka!




Kazi ya kikundi

mafunzo, mkufunzi wako atawapanga katika makundi ili kufanya kazi fulani maalum kwa pamoja.



Swali&Jibu

Kipindi cha Maswali na Majibu ni muhimu sana. Unahimizwa kuuliza maswali mengi ili kuhakikisha kwamba unaelewa kikamilifu shughuli mbalimbali za mafunzo.



Sehemu ya Vidokezo

Sehemu hii ni kwa ajili ya kuandika maelezo na kujipima mwenyewe juu ya yale uliyojifunza

KARIBUNI WAHOJAJI WA KUJITOLEA!

Kama Mhojaji wa Uwezo, wewe ni nguzo muhimu kwenye mchakato wa Uwezo, na ubora wa tathmini ya kujifunza ya Uwezo unategemea sana jitihada na umakini wako. Kwahiyo, ni muhimu uwe na uelewa mzuri wa mchakato na taratibu za tathmini ya Uwezo.

LENGO LA MWONGOZO HUU WA WAHOJAJI NI NINI?

- Kukupa uelewa wa kina kuhusu dhana na mchakato wa Uwezo ili uweze kuelezea wengine kwa usahihi.
- Kukuwezesha kufahamu na kuelewa mchakato wa tathmini ili uufuate na kutekeleza kwa usahihi.
- Kukupa ujuzi muhimu na kukuandaa kufanya zoezi la utafiti kwa usahihi katika ngazi tatu (ofisi ya kijiji/mtaa, shule na kwenye kaya).
- Kukupa uelewa wa jinsi ya kurekodi taarifa ulizokusanya kwenye kitabu cha utafiti
- Kukuandaa kufanya mahojiano na mwenyekiti/kiongozi wa kijiji kwa usahihi na kurekodi taarifa zilizokusanywa kwenye dodoso la utafiti wa eneo la kuhesabia.
- Kukuandaa kufanya zoezi la utafiti shuleni kwa usahihi na kurekodi taarifa ulizokusanya kwenye fomu ya utafiti shuleni.
- Kukuandaa kufanya mahojiano na mkuu wa kaya kurekodi taarifa zote muhimu kwenye dodoso la utafiti wa kaya
- Kukupa ujuzi muhimu unaohitaji katika kumpima mtoto, kupanga daraja na kurekodi matokeo ya watoto wote wenye umri wa miaka 6-16. Kukupa uelewa mzuri kuhusu maana ya mrejesho wa papo kwa papo na jinsi unavyotolewa.

SURA YA 1: KUHUSU UWEZO NA MCHAKATO WAKE



Kumbuka

Kama mhojaji wa kujitolea wa Uwezo, wewe ni balozi/ mwakilishi wa Uwezo kijijini kwako. Utapokelewa vema zaidi kwa kaya ikiwa unaweza kuongea kwa ujasiri na una ufahamu mzuri kuhusu Uwezo.


0.1 MALENGO YA SEHEMU HII NI NINI?

Sehemu hii itakuwezesha kuelewa kwa kina dhana ya Uwezo na kuwa na uwezo wa kuwaelezea kwa usahihi na kwa kujiamini watu utakaokutana nao kijijini, shuleni na kwenye kaya wakati wa mchakato wa tathmini ya mwaka ya matokeo ya kujifunza.

1.2 CHIMBUKO LA UWEZO NI NINI?

- Uwezo ni jitihada inayotekelezwa katika nchi za Kenya, Uganda na Tanzania ambayo ilianza mwaka 2009, kufuatia hamasa iliyotokana na Ripoti ya Mwaka ya Hali ya Elimu (ASER) huko India.
- Tathmini zinazoongozwa na wananchi za kuhusu ujifunzaji wa watoto, kama ASER na Uwezo, zinafanywa kila mwaka katika mabara 3 na nchi 9 duniani kote: Kenya, Tanzania, Uganda, India, Pakistan, Mali, Senegal, Nigeria na Mexico.
- Jitihada hizi huru katika nchi hizo zinatekelezwa kwa pamoja kama familia, kukusanya na kusambaza ushahidi kuhusu ujuzi halisi wa watoto katika kusoma na kufanya hisabati.
- Siyo kwamba wanashirikishana taarifa wao kwa wao tu, lakini pia wanatoa taarifa kwa wananchi, serikali za mitaa na kitaifa, na mashirika muhimu duniani kote yenye nia ya kuboresha kiwango cha kujifunza kwa watoto.

- Hadi sasa, jitihada hizi zimetathmini watoto zaidi ya milioni moja duniani kote. Ukanda wa Afrika Mashariki peke yake, takriban watoto 350,000 wanapimwa ujuzi wao wa kusoma na kuhesabu kila mwaka.
- Kwa pamoja, tathmini zinazoongozwa na wananchi zinashirikisha maelfu ya watafiti wa kujitolea kila mwaka. Katika Afrika Mashariki, zaidi ya wahojaji wa kujitolea 20,000 hutembelea kaya kila mwaka.
- Wewe ni sehemu ya jitihada hii, inayohusisha wananchi kushughulikia tatizo la ujifunzaji linalowakabili watoto wetu.



1.3 JITIHADA NI NINI?

Jitihada inafafanuliwa kama...

- Hali ya wananchi kutathmini tatizo katika jamii yao ambalo linawahusu, na kuamua kuchukua hatua ya haraka, kulitua tatizo hilo ili kujenga jamii bora

**Sehemu ya Vidokezo**

UNAFIKIRI 'Jitihada' maana yake nini? Je ni neno gani lingine rahisi unaweza kutumia kumaanisha "Jitihada"

1.4 UKWELI MUHIMU KUHUSU UWEZO

- Nijitihada inayoongozwa na wananchi
- Ni jitihada inayoratibiwa na Twaweza East Africa
- Ni neno la Kiswahili lenye maana ya umahiri/uwezo
- Inafanyakazi eneo la Afrika Mashariki (Kenya, Tanzania na Uganda)
- Inapima watoto ujuzi wa msingi wa kusoma na kuhesabu
- Inakusanya taarifa kutoka shuleni na kwenye kaya
- Inatekelezwa na wananchi kwenye jamii
- Inatia msukumo kwa wananchi kuchukua hatua kuboresha viwango vya ujifunzaji vya watoto wao
- Inataka kufahamu 'Je, watoto wetu wanajifunza?'

**Sehemu ya Vidokezo**

1.5 SIFA MUHIMU ZA UTAFITI WA UWEZO NI ZIPI?

Tathmini ya Uwezo ina vipengele muhimu vifuatavyo:

- Ni tathmini ya kikaya
- Ni tathmini ya kitaifa
- Inatumia zana rahisi ambazo ni rahisi kueleweka
- Inaendeshwa na wananchi wazalendo na hutumia wahojaji wa kujitolea kutathmini watoto
- Inatoa mrejesho wa matokeo papo kwa papo kwa mtoto na mzazi
- Inaangalia stadi za msingi za watoto kusoma na kufanya hesabu

Sehemu ya Vidokezo

Kwa kutumia point 5 hapo juu, elezea Uwezo kwa lugha yako asili au lugha utakayotumia kwenye kaya

**1.6 MALENGO YA UWEZO NI NINI?**

Uwezo inalenga:

1. Kutathmini stadi za watoto katika kusoma na kufanya hisabati kote nchini Kenya, Tanzania na Uganda
2. Kupata data za kuaminika na za kina juu ya viwango vya kusoma na kufanya hisabati kila mwaka
3. Kukusanya data ambazo ni mkusanyiko wa takwimu ngazi ya wilaya
4. Kutoa taarifa ya matokeo ya tathmini kwa mapana zaidi - kwa wananchi, wazazi, walimu na serikali
5. Kuchochea wananchi kuchukua hatua ili kuboresha viwango vya kujifunza vya watoto katika jamii zao



Kama unataka kuandika kumbukumbu zozote, tafadhali andika hapa

1.7 KILE AMBACHO UWEZO SIYO

Uwezo sio:

- Inafadhiliwa na serikali
- Chanzo cha kufikiri/mawazo
- Kikundi cha kushawishi
- Mfuko

1.8 MATOKEO YA UWEZO

Je, unajua?

- 1 Mtoto mmoja kati ya watoto watatu walioandikishwa katika Darasa la 3 nchini ndiyo wana uwezo wa kufaulu majaribio yote ya Kiingereza, Kiswahili na Hisabati yaliyoandaliwa katika ngazi ya darasa la pili
- 2 Hata katika darasa la 7, bado wastani wa watoto saba katika ya kumi ndiyo wana Uwezo wa kufaulu majaribio ya Kiingereza, Kiswahili na Hisabati ya ngazi ya Darasa la 2
- 3 Kwa wastani, walimu wawili kati ya kumi wanakuwa hawapo mazingira ya shuleni wakati wote

HABARI ZA ASUBUHI MZEE. JINA LANGU NAITWA SARA NA NI MTAFIGI WA KUJITOLEA WA UWEZO. UMEWAHI KUSIKIA KUHHUSU UWEZO HAPO KABLA? UWEZO NI

NA SIJUI UNaweza KUNIAMBIA, KAMA KIJIKI HIKI KINA..... KITHO CHA POLISI BARABARA YA LAMI..... MAJI YA UHAKIKA YA UMMA?

USIWE NA WASIWASI, HUU SI KAMA MTHANI WA SHULENI. TUPO HAPA KUBAINI JINSI UNAVYOWEZA KUFANYA VIZURI KATIKA MAJARIBIO HAYA MAFUPI



SURA YA 2: KUELEZEA MCHAKATO WA UTAFITI

2.1 MALENGO YA SEHEMU HII NI NINI?

Malengo ya sehemu hii ni kukuwezesha:

- Kufahamu umuhimu wa kupanga na kufanya maandalizi kwa ajili ya tathmini
- Kujua wapi na kwa utaratibu gani unatakiwa kukusanya taarifa zinazohitajika
- Kuingia shuleni na kwenye kaya kwa usahihi

KUSHUGHULIKIA KWA USAHIHI MATUKIO MBALIMBALI YA KAYA NA WATOTO UNAYOWEZA KUKUTANA NAYO.

2.2: UTARATIBU WA ZIARA

1. NGAZI YA KIJIKI:

1. Mtembelee Mwenyekiti wa Mtaa, siku ya kwanza ya Tathmini
2. Jitambulisha na kuwasilisha barua za utambulisho
3. Thibitisha Mkoa, Kata, Kijiji / Mtaa, Wilaya / Halmashauri, na namba ya Eneo la Kuhesabia (EA)
4. Kamilisha kujaza Fomu ya Taarifa za Eneo la Kuhesabia

2. NGAZI YA SHULE:

1. Tembelea Shule kabla ya kutembelea kaya
2. Tembelea ofisi ya mwalimu mkuu kabla ya kutembelea vyumba vya madarasa
3. Jitambulisha kwa mwalimu mkuu na uwasilisha barua za utambulisho
4. Kamilisha kujaza Fomu zote za data za shule na uchunguzi wa darasani

3. NGAZI YA KAYA:

1. Ziara ya kutembelea kaya inapaswa ifanywe mara tu baada ya Fomu ya Taarifa za Kijiji na Fomu ya Taarifa za Shule kuwa zimekamilika kujazwa.
2. Jitambulisha kwa mkuu wa kaya
3. Kamilisha kujaza Fomu ya Taarifa ya Kaya

Kumbuka

Hakikisha umemtembelea mwenyekiti wa kijiji/mtaa KABLA ya kuanza zoezi la tathmini



SURA YA 3: KUTEMBELEA SHULE

Kutembelea shule kunafuatia baada ya kutembelea eneo ya kuhesabia. Yaani baada ya kutembelea ofisi ya kijiji/mtaa.

3.1: KUJITAMBULISHA SHULENI




Kumbuka

JITAMBULISHE KWA MWALIMU MKUU KWANZA. MUONESHE BARUA ZA IDHINI YA KUFANYA UTAFITI

Hakikisha unaeleza yafuatayo:

“Uwezo inafanya shughuli za tathmini katika wilaya zote za Afrika mashariki. Shule hii imechaguliwa kwa sababu imo kwenye eneo la kuhesabia lililochaguliwa kwenye sampuli ya wilaya. Pia kaya ishirini katika Eneo hili la Kuhesabia zitatembelewa leo na kesho, na katika kaya hizo watoto wenye umri wa miaka 7-16, watafanyiwa majaribio ya kiwango cha darasa la pili. Sote tunakubaliana kuwa wengi wa watoto wetu wameandikishwa shuleni. Hivyo tunakusanya takwimu ambazo zitatusaidia kujibu swali “Je watoto wetu wanajifunza?” ”





S&J

Ni muhimu kumuuliza maswali mkufunzi kama huelewi vizuri au kama unahitaji ufafanuzi zaidi kuhusu kipengele chochote cha ziara ya kutembelea shule.

SURA YA 4: KUTEMBELEA KAYA

Ziara za kutembelea kaya lazima zifanywe baada ya kukamilisha taarifa za kijiji/mtaa na fomu ya utafiti shuleni. Unapaswa kujitambulisha kwa mkuu wa kaya na kisha kamilisha fomu ya utafiti kwenye kaya.

4.1: KAYA NI NINI?

Kaya ni kundi la watu **wanaoishi ndani ya nyumba moja kwa kawaida**. Watu hawa lazima pia wawe **wanapika na kula katoka chungu kimoja** ndipo waitwe ni watu wa kaya moja.



4.2: KUIINGIA KATIKA KAYA

Unapoingia kwenye kaya, zingatia yafuatayo:

1. Thibitisha kama hiyo ni kaya sahihi, kama ilivyoainishwa kwenye orodha ya kaya uliyopewa.
2. Jitambulisha kwa mkuu wa kaya. Unaweza kukaribishwa ndani au usikaribishwe ndani ni sawa tu
3. Kama hukukaribishwa ndani, tafuta sehemu nzuri nje kaa hapo
4. Tambulisha Uwezo (MUHIMU SANA) na eleza sababu za ujio wako.
5. Jibu maswali yoyote ambayo utaulizwa na mwanafamilia yeyote.
6. Omba ruhusu ya kuifanyia utafiti kaya hiyo. Ni lazima upate ruhusa ndipo uanze zoezi la utafiti kwenye kaya hiyo.
7. Sisitiza kuwa ni muhimu kwa wazazi kuangalia mchakato mzima wa tathmini maana utawapatia mrejesho mwishoni. (Hii ni muhimu sana).
8. Fanya mahojiano na mkuu wa kaya na wapime watoto wote wenye umri miaka 7 – 16
9. Pale ambapo watoto hawako nyumbani (wanaweza kuwa kijijini au kiwanjani), kuchukua taarifa zao; jina, umri na kama wanasoma au la. Muombe mwanafamilia akuitie mtoto ili uongee naye moja kwa moja. Kama mtoto amechelewa sana kuja, wekea alama kaya hiyo kisha rudi baadaye ukikamilisha kaya nyingine.
10. Fanya zoezi la kupima hali ya lishe (MUAC) kwa watoto wote wenye umri wa miezi 6 hadi miaka 14.
11. Pima madini joto kwenye chumvi
12. Toa mrejesho wa papo kwa papo kwa uaminifu kuhusu kuhusu ngazi za kujifunza za mtoto, pamoja na MUAC na chumvi.
13. Washukuru wanafamilia unapokamilisha zoezi la utafiti kwenye kaya

Kaya zinazohesabika katika utafiti	Kaya ambazo hazipaswi kujumuishwa katika utafiti
Kaya zisizo na watoto wenye umri kati ya miaka 3-16. (Taarifa kuhusu mkuu wa kaya bado zinapaswa kukusanywa.)	Mhojaji anapaswa kuripoti mara moja kwa mratibu wa wilaya anapokutana na kaya zifuatazo Nyumba ambazo zimefungwa kwa sababu wanafamilia wamehama kutoka katika eneo hilo au hawatarudi siku hiyo. Kaya hizo zinapaswa kurekodiwa kama “hakuna majibu”.
Kaya anayoishi mtu mmoja aidha mwanaume au mwanamke anakula kutoka katika jiko lake mwenyewe	Kaya ambayo imekataa kushiriki katika utafiti. Kaya hiyo inapaswa kujazwa “Hakuna jibu”
Kaya ambayo imefungwa au hakuna mtu aliyepo nyumbani lakini watarudi baadaye	Nyumba ambazo kuna watoto lakini hakuna watu wazima wa kutoa idhini kwa watoto kushiriki katika utafiti



Kumbuka

Haupaswi kubadilisha kaya yoyote iliyo kwenye orodha. Baada ya kufanya majaribio kadhaa kufanya utafiti kwenye kaya na ukashindwa kuipata kaya, unapaswa kuwasiliana mara moja na Mratibu wa Wilaya

SURA YA 5: KUWAPIMA WATOTO

Mara baada ya kumaliza kukusanya taarifa zote za kaya kutoka kwa mkuu wa kaya, unaweza kuendelea kuwapa majaribio watoto. Jedwali hapa chini litakuongoza kufanya maamuzi yanayohusu makundi tofauti ya watoto unayoweza kukutana nayo kwenye kaya.

Kumbuka

Watoto kutoka kaya zilizochaguliwa lazima wapimwe wakiwa nyumbani kwa kutumia sampuli ya majaribio uliyopewa. Hairuhusiwi kumpima mtoto akiwa shuleni au nje ya kaya.



Umri wa mtoto	Taarifa gani za kujaza	Kufanya majaribio?
Chini ya miezi 6	<ul style="list-style-type: none"> ● Usimuorodheshe ● Mjumlisha katika jumla ya idadi ya wanakaya 	● Hapana
Miezi 6 - miaka 6	<ul style="list-style-type: none"> ● Jina kamili ● Wasifu ● Mjumlisha katika jumla ya idadi ya wanakaya ● Pima mzingo wa mkono (MUAC) ● Wenye umri wa miaka 3-6 years, nakili taarifa za shule za awali 	● Hapana
Wenye umri wa miaka 7-16 ambao aidha <ul style="list-style-type: none"> ● Wako shuleni ● Wamewahi kuandikishwa shule hapo awali lakini wameacha 	<ul style="list-style-type: none"> ● Jina kamili ● Wasifu ● Taarifa za kusoma/elimu ● Pima MUAC 	● Ndio. Toa majaribio kwa watoto wote wenye umri wa miaka 7-16 kama wanasoma kwa sasa ama wamewahi kuandikishwa shule hapo awali
Wenye umri wa miaka 7-16 ambao kamwe hawajawahi kuandikishwa katika shule.	<ul style="list-style-type: none"> ● Jina kamili ● Wasifu ● Pima MUAC 	● Ndio. Mfanyie majaribio hata kama hajawahi kuandikishwa shule.
Zaidi ya miaka 16	<ul style="list-style-type: none"> ● Usimuorodheshe ● Usichukue wasifu ● Mjumlisha katika jumla ya idadi ya wanakaya ● Usimpime MUAC 	● Hapana. Usimfanyie majaribio mtoto yeyote mwenye umri wa miaka zaidi ya 16, hata kama bado anasoma shule.

Watoto walio kwenda nje ya EA yao:

Kunaweza kuwa na watoto kutoka kaya fulani ambao wamekwenda shule za bwani au kuishi na ndugu zao. USIWAORODHESHE hao. USIWAJUMUISHE kwenye idadi ya wanakaya.

Watoto waliokuja kutembelea ndugu zao:

USIWAPIME watoto ambao wametembelea ndugu au marafiki zao kwenye kijiji au kaya iliyochaguliwa. USIWAPIME watoto ambao hawaishi siku zote kwenye kaya hiyo, hata kama wataomba kupewa majaribio.

SURA YA 6: UFAFANUZI WA TATHMINI ZA KUSOMA NA HISABATI

6.1: JINSI YA KUTATHMINI WATOTO

Kabla ya tathmini, ni muhimu kufanya mazoezi ya kusoma kwa sauti maneno, aya, hadithi na maswali ya ufahamu kwenye lugha ya Kiswahili na kiingereza. Hii itakuwezesha kuwa na uzoefu an matamshi na majibu yanayotarajiwa. Hili ni zoezi ambalo linaweza kufanywa katika jozi wakati wa mafunzo.



Kumbuka

Hatuendi vijijini “kuchunguza” watoto, au kuwa watoa hukumu kwa makosa ya watoto. Tunakwenda kubaini kile ambacho watoto wanaweza kufanya BILA SHIDA katika stadi za kusoma na kufanya hisabati.

- Fanya mazungumzo ya kirafiki na mtoto kabla ya kumtathimini. Hii itasaidia kujenga mazingira huru kwake. Ni lazima umfanye mtoto ajisikie huru kabisa kuanza mchakato wa tathmini. Ni muhimu watoto wawe huru na wasiwe na wasiwasi juu ya kile wanachokwenda kufanya. Mara nyingi, familia na majirani hukusanyika karibu kuangalia nini mtoto anafanya. Kuzungumza na mtoto kirafiki kutasaidia awe huru na tayari zaidi kufanya majaribio.
- Kuwa na subira na wape watoto muda na nafasi ya kutosha kujibu maswali. Usimchagulie mtoto swali la kujibu.
- Kumbuka kwamba hausubiri kukamata makosa. Lazima utambue jitihada anazofanya mtoto kujibu maswali.
- Kwa majaribio yote ya kusoma na kuhesabu, anzia kutathmini ngazi ya chini na fuata maelekezo kwa makini zaidi. Maelekezo yote yako kwenye majaribio yenyewe.
- Amua kwa usahihi ni NGAZI GANI YA JUU mtoto amefikia bila shida.

6.1.1 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI WA KUMTATHMINI MTOTO

1. Mpe kila mtoto kwenye kaya jaribio lake tofauti.
2. Katika kila ngazi, mtoto watapewa nafasi 2 za kurudia kujibu maswali kabla ya kuamua ama kuendelea na zoezi au kuacha jaribio hilo
3. Watoto wataanzia ngazi ya chini kabisa kujibu maswali na kupanda juu hadi watakapofika ngazi ya juu kabisa kwenye kusoma au kufanya hesabu.
4. Mtoto atapangwa gredi kulingana na kiwango cha juu alichofikia. Maelekezo ya kupanga gredi yako sawa kwa watoto wote kama ilivyoelezwa kwenye kitabu cha utafiti.
5. Mtoto apewe kitabu akishike mwenyewe wakati anasoma
6. Usiweke maksi/alama kwenye kazi ya mtoto kuonesha kama amepata au amekosa. Unapaswa kuyajua majibu ya majaribio anayofanya mtoto.

6.1.2 KUPIMA UJUZI WA KUSOMA

1. **Ngazi ya silabi/neno/:** mtoto aruhusiwe kuchagua na kusoma machaguo 5. Na aweze kusoma kwa usahihi angalau machaguo 4 ili kumuweka kwenye ngazi hii. Mtoto apewe nafasi ya pili kujaribu tena kusoma maneno au silabi kama alishindwa mara ya kwanza kusoma machaguo 4 kwa usahihi.
2. **Ngazi ya sentensi/aya:** mtoto aruhusiwe kuchagua aya ya kwanza au ya pili kusoma. Wakati akisoma, aruhusiwe kufanya makosa mawili tu si zaidi. Akifanya makosa zaidi ya mara mbili apewe nafasi ya kujaribu tena kabla ya kuamua kama mtoto anaweza au hawezi kusoma aya.

3. **Ngazi ya hadithi:** mtoto aruhusiwe kufanya makosa si zaidi ya manne. Akifanya makosa zaidi ya manne apewe nafasi ya kujaribu tena kabla ya kuamua kama mtoto anaweza au hawezi kusoma hadithi.
4. Mtoto aambiwe ajibu maswali ya ufahamu kama tu ameweza kusoma hadithi kwa usahihi.

Tafadhali kumbuka:

1. Makosa ni pamoja na kuacha neno, kuruka neno au kusoma sentesi kwa kukata kata maneno.
2. Athari za lugha asili kwenye kutamka maneno **siyo kosa**.
3. Kama mtoto hawezi kusoma sentensi ya kwanza, mwambie mtoto asome tena. Kama mtoto hawezi kusoma kwa mara ya pili, mpange kwenye gredi anayostahili na endelea.
3. Ufahamu: mtoto ajibu maswali mawili baada ya kufanikiwa kusoma hadithi kwa usahihi. Mtoto anaweza kurejea kwenye hadithi kutafuta majibu.

6.2: MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

Swali: Ninapomsikiliza mtoto akisoma, kuna tofauti katika matamshi na sauti kutokana na lugha ya asili ya mtoto au lugha ya mama. Je, nichukulie tofauti hizi kama kosa?

Jibu: Hapana. Usichukulie tofauti hizi kama kosa. Mwambie mtoto asome tena kwa umakini.

Swali: Ninapomsikiliza mtoto akisoma, anaweza kusoma neno vibaya au kuruka neno. Je, nichukulie hili kama kosa na kumuweka mtoto katika kundi la daraja la chini?

Jibu: Hapana. Kama ilivyo hapo juu, mwambie mtoto asome tena kwa umakini. Aidha atasoma vizuri kwa usahihi au ataendelea kufanya makosa yale yale. Kama ataendelea kufanya makosa yale yale, kukosea maneno au kusoma neno lisilo sahihi, basi hii ina maana kwamba mtoto anapata ugumu.


wa kusoma katika ngazi hiyo na kwamba inapaswa awekwe kwenye ngazi ya chini.

Swali: Wakati anasoma aya au hadithi, inakuwaje endapo mtoto amefanya makosa 3 au zaidi?


Jibu: ngazi ya aya: Kama mtoto kafanya makosa 3 au zaidi, huyo hawezi kusoma aya. Muweke kwenye gredi ya maneno.

Ngazi ya hadithi: Kama mtoto kafanya makosa 5 au zaidi, huyo hawezi kusoma hadithi. Muweke kwenye gredi ya aya.

UFAFANUZI WA TATHMINI YA KUSOMA



UFAFANUZI WA TATHMINI YA HISABATI




SURA YA 7: KUPIMA MZINGO WA MKONO (MUAC)

7.1 MZINGO WA MKONO (MUAC) NI NINI?

Mzingo wa mkono, kwa Kiingereza *Mid Upper Arm Circumference (MUAC)* ni kipimo kinachowezesha kutambua kwa haraka hali ya afya ya lishe kwa mtoto na kubaini ikiwa

mtoto ana utapiamlo au la. Huwa ni kipimo kinachochukuliwa kwa kupima mzunguko wa mkono katikati ya kifundo cha bega na kiwiko cha mkono. Mwaka huu, Uwezo ingependa kubaini hali ya afya na lishe kwa watoto na uhusiano wake na uwezo wa watoto kujifunza nchini Tanzania.



7.2 JINSI YA KUPIMA MUAC

1. Muombe mzazi / mlezi wa mtoto kuwa unataka kupima hali ya lishe kwa kutumia kipimo cha mzunguko wa mkono.
2. Saidiana na mzazi kuhahikisha mkono wa mtoto wa kushoto hauja funikwa na nguo yoyote.
3. Mtoto akunje mkono wa kushoto na aulaze kwenye tumbo lake.
4. Tafuta kifundo cha bega na kiwiko cha mkono wa mtoto.
5. Pima urefu kutoka kifundo cha bega hadi kiwiko cha mkono.
6. Tafuta nusu ya kipimo na weka alama.
7. Chukua utepe au futi kamba na zungusha kwenye mkono sehemu iliyowekwa alama.
8. Hakikisha utepe haubani wala kulegea.
9. Soma mzunguko kwa kukutanisha utepe sehemu ya kati.
10. Soma mzingo wa mkono kwa kuangalia mishale iliyopo kwenye utepe.
11. Soma kipimo katika sentimeta 0.1 ya karibu na kurekodi sambamba na jina la mtoto lililoorodheshwa katika dodoso la Tathmini.

7.3 UTOAJI WA MREJESHO WA MUAC

Umri	Utapiamlo mkali	Utapiamlo wa kadiri	Hakuna utapiamlo unaotokana na lishe duni
Miezi 6-miaka 5	Chini ya sm 11.5	sm 11.5-12.4cm	sm 12.5 na zaidi
Miaka 5 -9	Chini ya sm 13.5	sm 13.5 hadi sm 14.4	14.5 na zaidi
Miaka 10-14	chini ya sm 16.0	sm 16.0 hadi sm 18.4	sm 18.5 na zaidi

USHAURI: Kama matokeo ya kipimo cha MUAC yanaonesha hali ya mtoto kuwa na utapiamlo, mshauri mzazi aonane na mtaalum wa afya haraka sana kupata ushauri.

SURA YA 8: KUPIMA MADINI JOTO KATIKA CHUMVI

8.1 MADINI JOTO NI NINI?

Madini joto mwilini ni muhimu katika hatua mbalimbali za ukuaji wa binaadamu na wanyama tangu kiumbe kikiwa tumboni hadi utu uzima. Athari za upungufu wa madini joto mwilini ni pamoja na udumavu, ulemavu, utaahira, mimba kuharibika, mtoto kufia tumboni au kufa akiwa mchanga, kuvimba kwa tezi la shingo (goita). Madini joto hupatikana ardhini, maeneo ya tambarare, mito na maziwa. Mtu anapata madini joto kwa kula chakula kilichopandwa au kupatikana kwenye maeneo hayo. Lakini kuna sababu mbalimbali zinasababisha madini joto yasipatikane kwenye vyanzo hivyo au yapatikane kwa kiasi kidogo ambacho hakitoshelezi kwa mahitaji ya binaadamu. Hivyo serikali ya Tanzania imeamua kuchanganya madini joto katika chumvi ili yawafikie watu wengi kwakuwa chumvi huliwa na watu wengi.

8.2 JINSI YA KUPIMA MADINI JOTO KATIKA CHUMVI

Upimaji wa chumvi ili kujua kama ina madini joto au hapana hufanyika kwa kutumia "test kit" ambayo ina vichupa viwili vidogo, kichupa cha kwanza ni *starch solution* (ina rangi nyeupe) ambayo hutumika kutambua kama chumvi ina madini joto au hapana. Kichupa cha pili kina *recheck solution* (ina rangi ya pink) ambayo ina uwezo wa ziada wa kuhakiki na kuthibitisha kama kweli chumvi haina madini joto.

Hatua:

1. Chukua chumvi kijiko cha chai weka kwenye chombo chochote kisafi.
2. Weka tone moja (unaweza kuweka mpaka matone matatu) la *starch solution* kwenye chumvi.
3. Angalia rangi ya chumvi kama imebadilika kuwa rangi ya zambarau au bluu. Kama chumvi imebadilika kuwa rangi ya zambarau

au bluu hii inamaanisha kuwa chumvi hiyo ina madini joto. Na kama chumvi haijabadilika rangi basi chumvi hiyo haina madini joto.

4. Kama chumvi haijabadilika rangi inawezekana chumvi hiyo ina madini joto, lakini kuna uchafu (*contaminants*) ambao husababisha *starch solution* ishindwe kutambua kuwepo kwa madini joto kwenye chumvi na hivyo kutobadilika rangi hata kama chumvi hiyo ina madini joto.
5. Hivyo chukua chumvi sampuli ile ile uliyochukua mwanzoni kwa mwenye kaya na pima kijiko kidogo cha chai.
6. Weka *recheck solution* kwenye chumvi nyingine uliyopima mara ya pili katika kaya hiyo hiyo na ya sampuli ileile ili kuhakikisha kama kweli chumvi hiyo ina madini joto au haina.
7. Angalia kama chumvi inabadilika rangi na kuwa ya zambarau au bluu baada ya kuweka *recheck solution*.
8. Kama chumvi imebadilika na kuwa rangi ya zambarau /bluu basi chumvi hiyo ina madini joto.

Kama chumvi haikubadilika rangi hata baada ya kuweka *recheck solution* basi chumvi hiyo haina madini joto.

SURA YA 9: MREJESHO WA PAPO KWA PAPO

9.1: MREJESHO WA PAPO KWA PAPO NI NINI?

Moja ya sifa muhimu ya Uwezo ni kutoa mrejesho wa papo kwa papo wa matokeo. Mrejesho wa papo kwa papo unahusu kutoa taarifa kwa wazazi na wahojiwa kuhusu matokeo ya utafiti kwenye kaya punde tu baada ya kukamilisha zoezi la kuwapima watoto.

Hata hivyo, kile wanakaya wanaambiwa na namna ambayo matokeo hutolewa ni vitu muhimu sana kuwafanya wazazi waelewe.

- Kutoa mrejesho wa papo kwa papo ni muhimu SANA.
- UNAPASWA kutoa mrejesho kwa uwazi na uaminifu kwa wazazi kabla ya kuondoka kwenye kaya
- USIWAAMBIE wazazi nini cha kufanya

9.2: USHAURI KUHUSU MREJESHO WA PAPO KWA PAPO

- Majaribio haya yameandaliwa katika ngazi ya Darasa la 2.
- Mtoto yeyote ambaye yuko ngazi ya juu zaidi ya Darasa la 2 anapaswa kuweza kufanya majaribio yote bila shida.
- Kama mtoto aliye ngazi ya juu ya Darasa la 2 hawezi kufanya majaribio ya Darasa la 2, unaweza kuwaambia wazazi kwamba mtoto hana ujuzi katika stadi za msingi za kusoma /kufanya hisabati. Kama hawawezi kufikia ngazi za juu kabisa, basi ni dhaifu.
- Usiongeze chumvi au makeke, kwa mfano: “Mtoto huyu ana akili sana na atakuwa profesa.”
- Kamwe usitoe ahadi za uwongo kuhusu uwezekano wa msaada kutoka Uwezo



Kumbuka

Kuna hatua tatu za kufuata unapotoa mrejesho katika ngazi ya kaya:

- 1 Matayarisho:** wakati wa utambulisho, inapaswa kuwatarisha wazazi kuwa watoto wao watajaribiwa na mrejesho kutolewa
- 2 Tathmini:** Wafanye wazazi kuwa sehemu ya tathmini kwa kuwaomba kutazama
- 3 Kujumuisha:** Baada ya majaribio, zungumza na mzazi

Kumbuka...

- **Maelezo ya awali**-Ni muhimu kuwaandaa wahojiwa kupokea mrejesho mwanzoni kabisa mwa mchakato-wajue kuwa watoto wao watapimwa na mrejesho utatolewa kuhusu uwezo wa watoto. Na zaidi, wahojaji watajadiliana na wazazi nini cha kufanya ili kuboresha elimu ya watoto wao.
- **Ukweli halisi** – Kuwa mkweli wakati wa kutoa mrejesho na epuka kutia chumvi au kusifia mno watoto.
- **Maongezi changamani** – Mrejesho unapaswa kuwa mazungumzo ya pande mbili na siyo maelekezo ya upande mmoja.
- **Udhabiti**—mrejesho unapaswa kutolewa kwa utaratibu unaofanana kwenye kaya zote zilizotembelewa.
- **Heshima** – Daima kuwa na heshima na washukuru wahojiwa baada ya mchakato kupeana mrejesho

MAJARIBIO YAMEANDALIWA KWA NGAZI YA MAZOEZI YA DARASA LA 2. ASHA ANASOMA DARASA LA 3, MAANA YAKE ANAPASWA KUWEZA KUKAMILISHA NA KUFALLU MAJARIBIO YOTE BILA SHIDA. ASHA ALIFALLU KWA NGAZI YA "HADITHI" KATIKA KUSOMA NA NGAZI YA "KUZIDISHA" KATIKA HISABATI. HII INA MAANA ASHA AMEFANYA VIZURI KWA KIWANGO KINACHOTARAJIWA



SURA YA 10: MASUALA YA KIMAADILI

10.1 MALENGO YA SEHEMU HII NI NINI?

Sehemu hii inawezesha wahojaji wa kujitolea:

- Kuelewa maadili ya msingi ya Uwezo na mwenendo unaotarajiwa kwa Wahojaji wa kujitolea
- Kuelewa masuala ya maadili ya kuzingatia wakati wa utafiti wa Uwezo
- Kuelewa makosa yanayofanywa mara kwa mara wakati wa kufanya tathmini ya Uwezo

10.2 VIWANGO/VIGEZO VYA MAADILI

Kama Mhojaji wa Uwezo, mwenendo wako katika jamii unapaswa kuendana na dhamira na maadili ya Uwezo. Baadhi maadili ya msingi ya Uwezo na tabia inatarajiwa na watu wote wanaofanyakazi na Uwezo imeelezwa hapa chini:

SIFA NA MAADILI YA UWEZO	TABIA YAKO
Uwazi	Daima kuwa mkweli: usitoe ahadi za uongo, usitie chumvi, usitoe majibu ya uongo kama unapata shida na maswali.
Si-kwa-faida	Usitoe wala kupokea zawadi yoyote, ikiwemo fedha, ili kuwapatia watu takwimu na ushahidi uliokusanya.
Huru na isiyogemea upande wowote	Usimpendelee yeyote katika jamii. Usitoe ushauri kwa shule na familia kupendelea ufumbuzi wowote wa njia ya watoto kujifunza.
Heshima kwa watoto na familia	Watendee watoto na familia kwa heshima, uvumilivu, na wema, bila kujali jinsi wao wanavyokutendea wewe.
Mawasiliano	Kama kuna jambo lolote kubwa, toa taarifa mara moja.

10.3 MASUALA YA KIMAADILI UNAYOPASWA KUTILIA MAANANI

1. Kila wakati omba ruhusa kutoka kwa mkuu wa kaya kabla ya kuanza utafiti
2. USIWAFANYIE majaribio watoto bila ridhaa ya mzazi au mlezi
3. Fuata hatua na kanuni zote kama zilivyoainishwa katika mafunzo
4. USIFICHUE majina ya watoto au wazazi, au taarifa zozote binafsi kwa wanakijiji
5. USITOE ahadi ya msaada wowote au ufadhili kutoka Uwezo. Wewe elezea tu kile kinachofanywa na Uwezo
6. USIBAGUE WATOTO. ULIZA MASWALI KWA WATOTO WOTE WALIO NA UMRI KATI YA MIAKA 7-16 KATIKA KILA KAYA.
7. Beba barua ya idhini ya kufanya utafiti wakati wote wa utafiti
8. Hakikisha unaripoti kwa Mwenyekiti wa Mtaa/Kijiji kabla ya kutembelea shule na kaya
9. Kama nyumba imefungwa, usichukulie unajua vyema taarifa za kaya hiyo na kuamua kujaza bila wahusika kuwepo
10. Kuwa mkweli katika mchakato mzima wa tathmini na epuka njia za mkato
11. Omba ridhaa kabla ya kupiga picha zozote

12. Wahojaji wa Kujitolea wanapaswa kuzingatia maadili ya kitamaduni wa jumuiya wanayokwenda kutembelea kwa mfano, namna ya kusalimia, kanuni za uvaaji wa jamii, nk
13. Kila mtoto/kaya inayoshiriki kwenye tathmini ina haki ya kupokea matokeo ya majaribio. Mrejesho ni haki


Kumbuka...

1. **Heshima** – Heshimu kila kaya unayotembelea.
2. **Kula vyakula** – Uwe makini unapokaribishwa chakula
3. **Kupiga picha** – Hakikisha unapata ridhaa kabla ya kupiga picha
4. **Vifaa vya Kielekroniki** – Jidhibiti kutumia vifaa vya kielekroniki muda wote uwapo kwenye zoezi k,v kupiga/kupokea simu, kutuma sms, kuchati *facebook* n.k
5. **Lugha** – Uwe makini na lugha unayotumia

6. **Adabu** - Daima heshima watu na washukuru
7. **Uvaaji** – uwe makini na uvaaji wako

10.4 MAKOSA YALIYOFANYWA MARA KWA MARA NA WAHOJAJI WA KUJITOLEA MWAKA 2014

1. Kushindwa kumtembelea mwenyekiti wa Mtaa au Afisa Mtendaji wa Kijiji (VEO)
2. Kaya inapokuwa imefungwa, walijaza baadhi ya taarifa na wasifu bila kumuuliza mkuu wa kaya
3. Kutowafanyia majaribio watoto wote wenye umri wa miaka 7-16 katika kaya
4. Kuwafanyia majaribio watoto wenye umri chini ya miaka 7 na zaidi ya miaka 16
5. Kutokutoa Mrejesho wa matokeo papo kwa papo
6. Kutorudi tena kufanya tathmini katika baadhi ya kaya ambazo watoto hawakuwepo wakati watathmini



SURA YA 11: KUHIFADHI TAKWIMU BAADA YA TATHMINI

11.1 JE, UNAKAMILISHAJE KARATASI YA MKUSANYO WA MAENEO YA KUHEMBA?

Baada ya kukamilisha tathmini na kabla ya kupeleka takwimu kwa Mratibu wa Wilaya, unahitaji kukusanya takwimu zote za kaya kwa kutumia karatasi ya mkusanyiko wa maeneo ya kuhesabia. Fuata hatua hizi kujaza takwimu kwenye karatasi ya eneo la kuhesabia.

- Kamilisha muhtasari wa kila kaya. Hii inapaswa kuingiza katika mstari chini wa fomu ya mkusanyo wa takwimu za kaya
- Hamisha muhtasari huu wa kaya kwenda kwenye karatasi ya mkusanyo wa takwimu za maeneo ya kuhesabia. Jaza kila kaya kwenye mstari tofauti.
- Kukamilisha muhtasari wa eneo la kuhesabia. Jumla ya eneo la kuhesabia iingizwe kwenye mstari wa mwisho wa karatasi ya maeneo la kuhesabia. Mpatia kitabu cha utafiti Mratibu wa Kijiji/Wilaya ukishakamilisha.

11.2 JINSI YA KUWASILISHA VITABU VYA TAKWIMU ZA UTAFITI?

Baada ya kukamilisha fomu zote za utafiti, ikiwa ni pamoja na mkusanyiko fomu EA, wewe kama Mhojaji wa Uwezo lazima ukague kwa makini taarifa zote ili kuhakikisha kuwa umefanya kila kitu kwa usahihi na umejaza taarifa kama inavyotakiwa. Kisha utapeleka vitabu vya utafiti kwa Mratibu Wilaya/Kijiji-ambaye naye:

1. Atachunguza vitabu vya utafiti ili kuhakiki ukamilifu wake na usahihi
2. Atafanya maamuzi kuhusu kitabu cha utafiti- atakipokea, kukiidhinisha kwa ajili ya utafiti wa marudio
3. Atawasilisha vifaa na vitabu vyote sekretarieti ya Uwezo ndani ya wiki 2 za kufanya utafiti
4. Atakupatia malipo yako ya kifuta jasho

RATIBA YA MAFUNZO

Muda/Tarehe	Mada
Siku ya 1:	
7:45 am – 8:00 am	Usajili
8:00 am – 8:30 am	kujitambulisha wahojaji wa kujitolea, matarajio na makubaliano ya Pamoja
8:30 am – 9:00 am	Kuitambulisha Uwezo (<i>Theory, group work & role plays</i>)
9:00 am – 9:30 am	Kufafanua Mchakato wa Utafiti Masuala ya Kimaadili katika mchakato wa Uwezo
9:30 am-9:50am	Kutembelea Eneo la Kuhesabia (Nadharia)
9:50 am -10:20	Kutembelea Kaya (Nadharia)
10.20-10:50 am Chai	
10:50am – 01:00 pm	Upimaji Watoto <ul style="list-style-type: none"> ● Ufafanuzi wa Tathmini ya kusoma Kiswahili na Kiingereza (soma kwa sauti seti zote nne za majaribio ya Kiingereza, Kiswahili na hisabati) ● Ufafanuzi wa makosa katika kusoma ● Masuala ya kimaadili katika upimaji wa watoto
1.00 - 2.00pm Chakula Cha Mchana	
2:00 – 4:50 pm	Ufafanuzi wa Tathmini ya kufanya hesabu (<i>Attempting all the sums in all samples</i>)
4:50 – 3:20 pm	Kupima uwezo wa macho kuona na maswali ya ziada
3:20-3:40pm	Kukusanya vitabu vya eneo la kuhesabia
3:40 – 4:10 pm	Mrejesho wa Papo kwa papo (<i>Household, school level</i>)
4:10 – 4:30 pm Chai na Kugawa vifaa	
4:30 – 6:30 WAHOJAJI WA KUJITOLEA KUTEMBELEA KAYA-MAFUNZO KWA VITENDO	
Day 2	
8:00am – 9.30 am	Mrejesho na Maswali yatoakanayo na ziara ya kutembelea Kaya
9.30am – 10:15 am	Kutembelea shule (Nadharia) <ul style="list-style-type: none"> ● Kujaza dodoso ● Kuwasilisha matokeo ya tathmini ya Uwezo
10.15 -10.45 am Chai na Kugawa vifaa	
10:45 AM – 1:45 PM WAHOJAJI WA KUJITOLEA KUTEMBELEA SHULE-MAFUNZO KWA VITENDO	
1:45 – 2:30 pm Lunch	
2.30pm – 3:20 pm	Mrejesho na Maswali yatoakanayo na ziara ya kutembelea shule
3:20pm –3:35 pm	Maswala ya kimaadili ya mchakato
3:35pm:4:45pm	Kugawa vifaa na taratibu za tathmini
4.45 pm Chai na Kufunga warsha	
Day 3	
8:00 Chai na Kusafiri kurudi vijijini	

Mwongozo wa Wahojaji

WA KUJITOLEA



Mtaa wa Mafinga,
barabara ya Kinondoni
S L P 38342, DSM, Tanzania
E: info@uwezo.net
www.uwezo.net